Watumishi wa KANU kupewa vitambulisho

KUANZIA SASA, Maafisa wa Chama cha K.A.N.U. na viongozi wa Kanu pamoja na vijana wanachudumia chama hicho watapatiwa vitambulisho rasmi, kuwasaidia kufanya kazi zao kwa urahisi.

na SAID BURHAN

Vitambulisho hivyo ambavyo vina alama ya chama cha Kanu na ni vya rangi nyekundu vitatumiwa na watumishi wote wa Kanu kwa kujitambulisha kwa maafisa wa serikali kwa mfano kama wakitaka kumtoa mtu kizuizini.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kanu tawi la Mombasa, Mhe. Shariff Nassir Tayeb ambaye pia ni Waziri Mdogo wa Biashara Mhe. Nassir, aliyasema hayo alipokuwa akihutubia mkutano malumu wa viongozi wa Kanu hapo katika afisi ya tawi hapo Majengo siku ya Alhamisi mnamo saa za alasiri.

Mkutano huo ambao ulihudhuriwa na viongozi wa ngazi zote za Kanu, pia ulihudhuriwa na Mbunge wa Mombasa Magharibi Mhe. Bwana Kioko.

Viongozi wote waliohutubia, walitilia mkazo upendano na mashirikiano baina ya viongozi mbali mbali wa chama cha serikali kwa maendeleo ya haraka ya mji wa Mombasa.

Na katika hafla ya kusherehekea siku kuu ya Jamhuri katika uwanja wa Manispaa ya Mombasa, Hotuba ya Rais ambayo ilisomwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bwana Luka Galgalo, ilifatiwa na hotuba ya Meya ambaye alieleza plani za kuimarisha huduma za Manispaa ya Mji wa Mombasa.

Alishangirwa sana aliposema kwamba hivi sasa mipango yatayarishwa ya kwenda kumuona Rais Moi kwa madhumuni ya kupendekeza wenye aridhi wawauzie wenye nyumba viwanja ili uskwata uondoke kabisa hapa Pwani.

Mbunge wa Mombasa Kaskazini Mhe. Bwana Said Hemed akihutubia wananchi waliomsikiliza kwa makini alishangazwa na kuona kwamba kuna mtindo wa kuajiri wafanyi kazi kutoka Bara kufanya kazi Mombasa japokuwa kazi yenyewe haihitajii elimu wala ujuzi.

Alisema kwamba hasemi hayo kwa kuonesha ukabila au kwa kupinga kabila fulani isandikwe kazi hapa Pwani.

KWA UFUPI

KRISMASI

MEYA wa mji wa Mombasa Diwani Rajab Sumba mwaka huu ataongoza sherehe za kuwasha mti wa Krismasi hapo "Treasury Square" tarehe 22 mwezi wa Decemba. Sherehe za mwaka huu zitatanguliwa na dansi muruwa (Mayor's Ball) siku ya Jumamosi tarehe 20 katika hoteli ya Oceanic ambapo kwenye hafla hiyo hayo, kutakuwa na maonyesho ya mishoni ya mavazi yatakayoandaliwa na "Tototo Home Industries". Tikiti za kuingilia katika sherehe zote mbili pamoja ni shillingi ishirini pekee ambazo pia zitatumiwa kwa mchango wa Mti wa Krismasi.

WALIMU

MMOJA katika viongozi wa Chama cha Walimu Bw. Amros Adongo mwaka huu huu huko Brazil, alichaguliwa kama Makamo Rais wa W.C.O.T.P. (Baraza la Ulimwengu la Kazi za Waalimu) ambayo ni heshima kubwa kwa mwalimu wa Kenya. Yaani ulimwengu unatambua bidii na heshima ya mwalimu wa Kenya.

Na katika ukarimu na upendo wa Rais alipotaka kuthubitisha ule msemo wa Kiswahili kwamba "Mchenza ngoma kwao hutuzwa" Mhe. Rais aliwatuza mawaziri na viongozi wengine wa nchi hii Nishani za Heshima kama kuonyesha furaha yake kwa kazi zao za kujenga Taifa hili. Katika hao viongozi waliopata Nishani hizo, tumewaona viongozi wawili wa walimu Bw. A. A. Adongo na Bw. David Mulindi.

SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku La Posta 87270, Mombasa KENYA

MUSIJITENGE NA SHEREHE ZA SERIKALI

NAOMBA nafasi katika gazeti lako nitoe malalamiko yangu kuhusiana na mahudhurio ya wananchi katika sherehe za Kiserikali kama vile siku kuu ya Jamhuri ambayo si ya kuridhisha hata kidogo.

Jambo hili linavunja moyo sana na hasa ukitazama kwamba Serikali ya Kenya chini ya Uongozi imara wa Bw. Daniel Arap Moi haimbagui mtu wa kabila lo lote au rangi yo yote bora tu anatii sharia za nchi hii.

Watu wote wana uhuru wa kufanya biashara zao na kuabudu dini zao na kuandaa sherehe za mila zao bila ya kuingiliwa na serikali bora waende mwendo wa kisawa sawa. Basi ni jambo gani linalomzuia mtu kuhudhuria katika hafla ya kiserikali kwa masaa machache tuu?

Kuhudhuria sherehe kama hizi ni kuipa heshima serikali yetu kwa yote yale ambayo inatufanyia hata tukaweza kuishi salama usalimini katika nchi hii. Jee wanadamu hawana shukurani hata ya kwenda uwanjani tu.

Kila aliyehudhuria sherehe za Jamhuri za hivi juzi, alijionea mwenyewe ile idadi ndogo ya watu waliohudhuria hali Mombasa ina makabila mengi ya watu lakini yaliyofika uwanjani ni mawili au matatu.

Na Madisii wetu wapya pia wamefanya kusahau kwamba utaratibu wa kuleta watu wengi uwanjani ni maandamano ya maidara na wizara, makampuni na viwanda. Na pia chama cha K.A.N.U. chataka kiitishe mkutano wa viongozi wa madhehebu mbali mbali ili hawa walete watu wao katika sherehe hizi.

Utaratibu huu ukifatwa watu wengi zaidi watahudhuria na haitaonekana kwamba hafla hiyo ni ya watu fulani tu peke yao. Huu si utumwa ni kuionesha serikali imani yetu.

Moh'd Ali Moroa,
Guraya, MOMBASA.

ULEVI NI ULEVI TU

SHUKURANI zote zimthubutikie Mwenyezi Mungu alo tuletea sharia ju ya halali na haramu, na akatuletea Mtume Muhammad alo tajwa ndani ya tarati na injili kua atawahalalishia umma wake yalo mazuri na kuwa harimishia yalo machafu.

Nauliza ndugu zangu jee hii ulevi ina kiwango maalum ambacho ukinywa hua si haramu??

Ni fahamuvyo mimi kua dini zote zina harimisha tembo na khaswa dini ya Kiisilamu ndio ulio tilia mkazo zaidi ju ya jambo hili.

Na Mwenyezi Mungu amesha uweka wazi uharamu wake, na ziko hadithi nyingi za Mtume ju ya kuharimishwa kwa ulevi na moja ni hii inayosema (kila kinacho levya ni tembo na kila tembo ni haramu) na kadhalika alisema "Mungu hakujaalia uzima wa umma wangu katika alicho kiharimisha".

Hii niufupi yakutujulisha tembo ni haramu iwe ni nyingi au kidogo, iwe kwa dawa au mengineyo. Umuhimu kua ni haramu.

Leo nashangazwa kusoma katika *Daily Nation* ya tarehe 17/9/1980 kua Saudi Arabia inaagiza Dry Beer kutoka Danish Brewery (Carlsberg) nchi ambayo Alcohol ni marfuku. Hapo hapo wakasema ina ladha kama beer lakini ina kipimo cha 0.05 ya Alcohol ambayo imekubaliwa na nchi hiyo ya Saudi Arabia.

Nataka kujua jee nikinywa chupa tano ya beer hiyo nitakua bado sijafikia kiwango cha uharamu?? Na ikiwa hiyo .05 yenyewe ina athari kwa nini wameikubali??

Nailhali yajulikana wazi kitu hicho kitafika Makka na Madina pia itafika na itatumiwa kote kote au itakua ni marfuku Makka na Madina?

Jee hii inamaana kua ulevi unaletwa kidogo kidogo katika hiyo nchi tukufu ya Makka na Madina?

Mungu atulinde na zama hizi inayojulikana kama ulimwengu wa utamaduni na maendeleo. Hakuna utamaduni au maendeleo kwa kitu alicho kikataza Mwenyezi Mungu, Maadamu tembo ni haramu basi ni harambu tu hakuna mabadiliko katika mari ya Mola.

Shariff M. Hashim,
MOMBASA.

WAZIRI MDOGO wa Biashara Bw. Shariff Nassir akiwa kama Mgeni wa Heshima katika sherehe za kuchangisha pesa kwa Umoja wa Kanyadoto huko Nairobi anaonekana akimkabidhi Waziri wa Mambo ya nje Dr Ouko (kushoto) mchango wake wa Shs. 10,000.

PICHA: KENYA NEWS AGENCY

Udugu wa Afrika Mashariki urudishwe tena

NCHI YA Uganda sasa imeshapata Raisi aliyechaguliwa kwa kura. Siku ya Jumatatu, iliiraukia nchi ya jirani ya Uganda na Kiongozi wa kuchaguliwa kwa kura za wananchi. Bwana Apollo Milton Obote akaapishwa kama Rais baada ya kuishi uhamishoni kwa miaka minane. Chama cha Obote, U.P.C. kilipata idadi ya viti na kile cha mpinzani wake yaani D.C. viti 44. Wachunguzi wa nchi za nje waliokuja mahususi kuangalia uchaguzi huo iwapo umeendeshwa kihalali, walipendekeza kwamba kulikuwa na uhalali wa kutosha katika uchaguzi kulinganishwa na hali ya Uganda.

Sisi majirani wa Uganda twaomba salama. Twawaombea wananchi wa Uganda wapate serikali itakayowaendesha kwa njia ya usalama na kuwachungia haki zao na mali zao kama inavyofanya serikali yetu ya Kenya chini ya uongozi wa busara wa Rais wetu Mhe. Bwana Daniel Arap Moi. Twapenda tuishi kwa amani na majirani zetu.

Tuna sababu kubwa ya kutaka amani na majirani zetu. Upande mmoja ni ndugu zetu. Makabila yote yanayoishi mipakani mwa nchi za Kenya, Uganda na Tanzania, yaligawanywa na wakoloni na japokuwa ni watu wamoja lakini walitawaliwa huku wakiwa wanaishi katika nchi mbali mbali. Mfano wa makabila hayo ni kama: Waluo, Wateso, Maasai, Wadigo na pia makabila haya yafuatayo, nusu yako katika nchi za Afrika Mashiriki na baadhu yako nchi nyengine za Afrika. Kwa mfano: Wagalla, Wamadi, Wabahima na Wayao.

Kwa hivyo tuna dharura za kiwanadamu za kuitisha salama na amani na majirani zetu. Masumbuko ya majirani zetu ni mateso kwetu pia. Serikali yetu ilidhihirisha jambo wakati ilipokuwa na vita vya maneno na Uganda. Juu ya kujibizana maneno makali lakini Kenya haikuwacha kupakuwa na kusafirisha mali ya Uganda ambayo hupitia bandari ya Kilindini Mombasa.

Watu wengine wanafikiri kwamba utawala mpya wa Uganda iwapo utafanikiwa kudumisha amani, basi misafara ya magendo itapungua sana. Kwani sababu moja ya kufanya magendo, jamaa hutaka chakula hicho kifike nchi jirani ili kikanufaishe jamaa zao ambao pengine wengekufa kwa njaa. Lakini iwapo uhusiano wa nchi hizi utazidi kurudufishwa na maongozi mapya ya Uganda, tuna tamaa kwamba mikataba ya biashara itazingatiwa kwa kikamilifu na hivyo iruhusu biashara ya halali iendelee bila ya kuafanya mgendo.

Magendo huletwa na upungufu wa bidhaa. Uganda si nchi masikini. Lakini tufani na dhoruba za kisiasa hazikuwezesha wakulima, wafanyikazi na wataalamu kuweza kuzalisha mazao ya kutosha. Obote amesema kwamba katika hatua zake za mwanzo za kurudisha hali ya uchumi ya Uganda ni kuzingatia kilimo.

Hatua ya Uganda kupata maongozi mapya ya demokrasi na tamaa ya wakaazi wa Afrika Mashariki kwamba itarudisha upendano wa asili wa nchi hizi kisiasi na kiuchumi na tamaa yetu kubwa ni kufunguliwa kwa mpaka baina ya Kenya na Tanzania.

COASTWEEK ★ ★ ★ ★ KARAMSHI HARJI

SHARP EL-211
Electronic Calculator
Coast Agents:
KARAMSHI HARJI
Box 81777 Tel: 312373
MOMBASA

SWAHILI CROSSWORD NO. 107



JINA..............................

SANDUKU LA POSTA..................

....

KWENDA KULIA:
1. Mto wa Zambia
5. Kiungo cha kukataa
6. Kuwa baridi
7. Aina ya embe
8. Ama
10. Rafiki
11. Juhudi, ghera
12. United Kingdom
14. Teketeza
16. Si P.M.
17. Medical Officer

KWENDA CHINI:
1. Sumbua, babaisha
2. Ni mdudu kisha ni nguo
3. Zaidi
4. Kiungo cha maneno
5. Kivazi cha kike
9. Uza imepungua
13. Ngapi?
15. Ala, jalada

Mshindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 106

S. Ali Attwas, Sanduku la Posta 80306, Mombasa.

Mshindi aombwa afike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 106 —

KWENDA KULIA:
4. MAKUBADHI, 6. UIMBAJI, 7. MEA, 8. DHIHAKA, 11. YA, 12. NINGA, 13. MAWE, 14. HASAMA.

KWENDA CHINI:
1. MUUNDI, 2. KAMBI, 3. BWANA, 4. DAIMA, 5. ISHARA, 9. HONGA, 10. KWAMA, 11. YOWE, 12. NOA

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Mshindi wa kwanza kila baada ya wiki mbili atapata zawadi ya Sharp EL-211 Electronic Calculator. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na KARAMSHI HARJI Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 31.12.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.

MBUNGE WA Kwale ambaye pia ni Waziri Mdogo wa Nguvu Mhe. Bwana K. Mwamzandi alikuwa Mgeni wa Heshima katika Harambee ya kuchangisha pesa kwa ujenzi wa Shule ya Kombano ambapo zaidi ya Shs. 13,000 zilikusanywa. Pichani wanaonekana Diwani Omar Chango na mwana biashara Kizindo wakitoa michango yao kwa Bwana Mwamzandi.

PICHA: COASTWEEK